

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA



MKOA WA SINGIDA:

ded.mkalamadc@singida.go.tz

Simu Na. 026 2924000

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
S. L. P. 1007
MKALAMA

TAARIFA KWA UMMA NA VYOMBO VYA HABARI

Afisa Mtendaji wa kata ya Kinampundu Wilayani Mkalama Ndugu Richard Laizer kwa niaba ya Msimamizi Mkuu wa Uchaguzi wa Jimbo, amemtangaza aliyekuwa Mgombea udiwani kupitia **Chama Cha Mapinduzi (CCM)**, ndugu **Marmo Sylvester Yambi** kuwa mshindi halali wa uchaguzi wa nafasi ya Udiwani wa kata hiyo ulifanyika tarehe 22/01/2017.

Yambi ameibuka mshindi wa uchaguzi huo baada ya kufanikiwa kupata kura 1,409 akifuatiwa na aliyekuwa Mgombea wa nafasi hiyo kupitia **Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)** ndugu **Mapokela P. Wazael** aliyejepata kura 804 huku Mgombea mwagine wa nafasi hiyo ndugu **Erick Ally Hamisi** kupitia **Chama cha Wananchi (CUF)** akishika nafasi ya tatu baada ya kupata kura 41.

Kwa Mujibu wa **Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC)**, idadi ya watu walioandikishwa kupiga kura katika uchaguzi huo ni **4,151** ambapo waliofika kupiga kura walikuwa ni **2,323** huku kura halali zilizopigwa zikiwa ni **2,254** na zile zilizoharibika zikiwa ni **69**.

Uchaguzi huo ulifanyika ili kuziba nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa diwani wa kata hiyo **Mhe: Hellena Kitila** aliyefariki tarehe 27/07/2016.

Ommary S. Mtamike
Afisa Habari (H/W)
MKALAMA
23 Januari, 2017.